

Ufahamu wa Kuhukumu

Mtunzi

Prof. Abdul Fatah Abdul Ghaniy Al-Awary

Mkuu wa Kitivo cha Masomo ya Misingi ya Dini

Kimetolewa na

Prof. Muhammad Abdul Fadhil Al-Qusy

Mjumbe wa Baraza kuu la Ulamaa
Makamu Mwenyekiti wa Taasisi

Kimefasiriwana

Ust. Ahmad Khalaf

Kihakikiwa na

Ust. Fadhili Mansour

Kimepitiwa na

Dkt. Sameh Anwar Bayoumi

Jumuiya ya Kimataifa ya Wahitimu wa Al-Azhar

Mradi wa kupinga mitazamo mikali -

mfululizo wa kupinga mitazamo mikali (6)

Msimamizi Mkuu
Prof. Muhammad Abdul Fadhil Al-Qusy
Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi wa Mradi
Usama Yasin
Mkurugenzi Mkuu wa Mradi
Hamdullah As-Safty
Namba ya usajili: 26643/2018
Namba ya Kimataifa: 978-977-85462-9-3

Tahadhari

Haki zote zimehifadhiwa na Jumuiya ya Kimataifa ya Wahitimu wa Al-Azhar Al-Sharif, hairuhusiwi kusambaza au kurudia kusambaza, au kutengeneza kitabu hiki au sehemu ya kitabu, au kukihifadhi kwenye vyombo vya uchapishaji pasi na kutangulia kuwepo makubaliano kwa maandishi na Jumuiya.

Jumuiya ya Kimataifa ya Wahitimu wa Al-Azhar

Mradi wa Kupinga Fikra za Misimamo Mikali

Chuo Kikuu cha Al-Azhar, Nasr City, Cairo, Arab Republic of Egypt

Namba ya Simu: +202 – 23868114

Fax: +202 23868116

Email: info@waag-azhar.org

Tovuti: www.waag-azhar.org

Kwa Jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema
Mwenye Kurehemu

Utangulizi

KWA UANDISHI WA PROF. MUHAMMAD ABDUL FADHIL AL-QUSY

MJUMBE KATIKA BARAZA KUU LA ULAMAA LA AL-AZHAR AL-SHARIF

Katika kitabu chake chenye utajiri wa maana na sura za kufikirika “Funguzi za Makkah” anasema Sheikh Mkuu “Muhyiddin Ibn Araby” kuwa: nafsi ya kweli ya Mwislamu: Haiwezekani kuwa hivyo pale yanaposimama makuzi yake ya nguvu ya ndani ya uelewa kwa kutoongezeka, basi ni lazima nafsi hiyo - katika mahusiano yake na ulimwengu pamoja na Muumba wa ulimwengu kupanda na kuongezeka kiroho kutoka hali ya kushuka kwa nguvu ya uelewa na kwenda kwenye hali nyengine iliyo juu zaidi, kinyume na hivyo nafsi hiyo itaendelea kuwa chini ya utawala wa mgando na kudumaa na kuwa rafiki wa usingizi na kifo!!

Kwa “Kupanda huku Kiroho” hukunjua peo zisizo na mwisho za nafsi ya mwanadamu, na viumbe vyote - kwa nafsi hiyo - vinakuwa vyenye uhai, huongea na Muumba wake pasi na ulimi, na kumsujudia bila ya mwili, pamoja na kuona ulimwengu kwa jicho la uzuri na upendo, roho na utulivu, hivyo humiliki kwa sifa hizo ulimwengu mzima na yaliyomo ndani yake yanayoonekana na yasiyoonekana.

Lau mtazamo huu wenye kuonekana ungechanganyika na sura ya Uislamu katika zama zetu za hivi sasa - basi ingekuwa ni kama kitendo cha uchawi katika utulivu wa nafsi yenye kiu ya haki na tumaini la usalama na uadilifu, ingekuwa ni tiba ya maradhi mengi ya zama na matatizo yake, na kugusa njia yake ya kwenda kwenye vifua na akili kuangazia nguvu ya giza na weusi wake usiochanganyika na rangi nyingine!!

Lau mtazamo huu wenye kuonekana ungechanganyika na sura ya Uislamu katika zama zetu hizi, basi usingewakuta Waislamu isipokuwa ni watu vifua vyao vimekuwa na utulivu na huruma, wakisameheana msamaha mzuri, wikipata maumivu ya kuugua kwa wafiwa na maumivu ya wanyonge, na wakiwa juu ya vitimbi vya chuki na ubaya wa kinyongo na tabia mbovu, hawaoni kwa mwanadamu ndani ya zama zote isipokuwa nyoyo zikidondokea kwenye haki, na kupumzika kwa uzuri wa uadilifu na tamania la misingi bora pasi na matumizi ya nguvu yenye kuua, wala chuki mbaya, wala damu kumwagika au viungo kutawanyika au vichwa kukatwa!!

Lakini mtazamo huu mwepesi wenye kuonekana ambao unachanganyika na hisia za busara - kwa masikitiko - umebadilika katika zama zetu za sasa kutoka kinyume kwenda kinyume, bali kutoka utofauti kuwa tofauti... basi upo wapi huo mtazamo ndani ya taswira nyembamba ambayo watu wake wamehiyarishwa kuwa “Uislamu” kwa ujumla wake ukubwa wake na huruma zake umejisogeza na kujiingiza kwenye “Matamania ya upendeleo binafsi wa mamlaka” na kujihusisha katika “Kujitumbukiza” kwenye usimamizi wa utawala, na Uislamu kwa - Watu hawa - umekuwa ni wenye kujikita na kujitenga kwenye “Mchezo wa Kisiasa” ambapo ni mazoezi na michezo, na kuondoka na mawimbi ya upepo peo zake na malengo yake makuu.

Upo wapi huo mtazamo kutokana na tabia zao mbaya ambazo zimepasua ulimwengu makundi mawili “Kundi” la imani ambayo haikimbiliwi isipokuwa na watu wa kundi hilo tu, na “Kundi” la ukafiri wa kijinga ambao hakuna jukwaa la kuuondoa na kumalizana nao, kisha watu wake - kwa mujibu wa mchezo wa kisiasa - wameanza kutembelea duniani kwa uharibifu na umwagaji damu, baada ya kuwaongoza vijana wengi wa Umma kwenye kuleta uadui na kuwaingiza kwenye shimo la kero, kisha wakawaacha wakipulizia moto wa vitendo vya nguvu na moto wa maangamizi, wakiwa na ari ya madaraka, na kukimbilia kwenye kiti cha mamlaka, na kuonja makazi ya utawala, kama kwamba hakuna kilichobakia katika “Uislamu” wote - roho maadili na misingi - isipokuwa ni “Mamlaka” yanayonyemelewa na “Utawala” wa kujipandisha, na “Uongozi” wenye kudharau roho za viumbe na kuruhusu kumwaga damu.

Upo wapi huo mtazamo kutokana na hao ambao wanajinasibisha na “Usalafi” na kudai kuwa ndio warithi wake, kisha wanaufanya kuwa ni sitara ya udanganyifu pindi wanapojumuishwa kwenye utasa wa kifikra pamoja na chuki na mitazamo ya upande mmoja, mpaka wakaingiza umuhimu wa Waislamu katika maumbile yaliyoingizwa kutoka nje, na mandhari ambazo zimefungua mlango - ulioegemewa baada ya hapo - na walinganiaji ugaidi, hapa ninamaanisha kile kinachoitwa katika fika zao zenye kuzunguka “Vita vya kundi lenye kuzuiliwa”, wazo ambalo linakaribia kuwa shari yenye kujikita kimakubaliano na makundi mengi ya matumizi ya nguvu hapo zamani na hata hivi sasa.

Upo wapi huo mtazamo kutokana na makundi ya kigaidi yenye majina ya chuki ambayo yamekuwepo ndani ya zama zetu hizi yakijiingiza kwenye udanganyifu na uzushi kwa jina la Uislamu na utawala wa Kiislamu, kisha walinganiaji wake hufanya uharibifu duniani kwa vitendo vya mauaji na mateso, pamoja na kukata shingo za watu mbele ya jicho la ulimwengu, pasi na kufumba jicho wala kugonga mioyo yao, bali pasi na kujitokeza kwa watu wao walioganda kifikra kuona kiwango cha uhalifu ambao wameusukumia

kwenye haki ya Uislamu pale walipokutanisha sura yake na sura ya umwagaji damu bali pindi walipoubadilisha “Uislamu” kwa athari za vitendo vyao hivi - katika mtazamo wa wengi - kuwa ni janga lenye kupiga ulimwengu mzima, na nini kinakuwa katika “Sura ya Kiakili” ambayo imejikita kwenye kumbukumbu za “Watoto Ulimwenguni” kuhusu “Uislamu” ambao wanadai kuulingania na kuinua bendera yake pamoja na kuinua neno lake?

Kisha hawa watu na hao hawaangalii kuwa matokeo ya “Jihadi ya Kiroho” ya Kiislamu katika mwelekeo tofauti yanapaswa kumuinua binadamu kwenye peo za juu kiroho, kiakili na kwa nguvu za ufahamu, yanayomhamasisha mwanadamu kwenye kuimarisha matunda yake kwa wenye njaa walio uchi na wagonjwa, kuimarisha tonge la kuishi na kiwango cha dawa, kunyoosha maisha na kumsukuma kwenye kumaliza ubinafsi mbaya ambao ni zao la ustaarabu wa manufaa ya vitu?

Huenda katika mfululizo huu wa kielimu tunajaribu kurudisha haki sehemu yake, na kufafanua kile kilichobandikwa na watu hao kwenye Uislamu ikiwa ni miongoni mwa mambo yanayoleta shaka na kusababisha makosa, ili kuwaonesha vijana ukweli wa Uislamu, na yanayopaswa kuwa nayo katika mwelekeo wao kwenye kupata radhi za Mola wao na kumfuata Mtume wao S.A.W.

Mwenyezi Mungu tunamuomba uwezesho na kukubali, Yeye ndiye Mbora wa kuombwa na kwake ni kwenye matumaini yote.

Kuhukumu (Hakimiya)

Miongoni mwa kadhia zilizo na ulazima kuziweka wazi ili tuweze kuwachukua vijana wetu na kuwaweka mbali na upotoshaji wa wajinga na fikra za wanaotaka kubadilisha haki pamoja na ufafanuzi wa wajinga: nayo ni kadhia ya “*Aya za kuhukumu kwa Alivyoteremsha Mwenyezi Mungu*” ambapo inahitajika kuainisha ufahamu na maana yake sahihi, na nimeelezea kwenye utafiti huu kwa sura ifuatayo:

Sehemu ya Kwanza: Kuhukumu katika lugha na kimsamiati.

Sehemu ya Pili: Matumizi ya neno kuhukumu kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Sehemu ya Tatu: Je! Inafaa kutumia neno kuhukumu kwa mwanadamu yeyote?

Sehemu ya Nne: Ufahamu wenye makosa wa Aya za kuhukumu kwa vile Alivyoteremsha Mwenyezi Mungu, na uchambuzi wa ufahamu huu, na mjadala wa watu wake.

Mwenyezi Mungu ndiye Muwezes haji na ndiye Msaidizi

Sehemu ya Kwanza :Ufahamu wa Kuhukumu Kilugha na Kimsamiati

Kuhukumu kwa upande wa lugha

Kuhukumu ni neno linalotokana na hukumu na asili yake ni kuzuia, amesema Ibn Faris kuwa kwenye herufi za Kiarabu: “Herufi *haa* (ح), herufi *kaaf* (ك) na herufi *miim* (م) ni zenye asili moja nayo ni kuzuia, na hukumu ya kwanza nayo ni kuzuia kutokana na dhuluma”⁽¹⁾.

Na hukumu: Ni elimu na ujuzi. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: **﴿Nasi Tulimpa hekima angali mtoto﴾**{Maryam, 12}. Kwa maana tulimpa elimu na ujuzi.

Na hukumu: Ni kutoa hukumu, husemwa amehukumu kati yao, kwa maana ametoa hukumu.

Na mada ya hukumu: Inatokana na umadhubuti, inasemwa kwa mfano, nimehukumu kitu, kwa maana ya nimefanya kinadhubuti⁽²⁾.

Kuhukumu kimsamiati:

Inamaanisha: Chanzo cha hukumu ya Sharia ya Kiislamu kwa watu wote ni Mwenyezi Mungu Mtukufu peke yake.

Qurani imeweka wazi hilo katika Aya zake nyingi kama vile katika kauli ya Mola Mtukufu: **﴿Hapana hukumu ila ya Mwenyezi Mungu. Yeye Anasimulia yaliyo kweli; naye ni Mbora wa kuhukumu kuliko wote﴾**{Al-An’aam, 57}.

Wanachuoni wa elimu ya Misingi ya Dini - katika utafiti wa mtoa hukumu - wamesema: Hakika mwenye kutoa hukumu na kutunga Sharia ni Mwenyezi Mungu Mtukufu peke yake hana mshirika.

Al-Amidy *Rehemea za Mungu ziwe kwake* amesema: “fahamu kuwa hakuna mwenye kutoa hukumu isipokuwa ni Mwenyezi Mungu Mtukufu, wala hakuna hukumu isipokuwa ile Aliyoitoa kuhukumia”⁽³⁾.

Imamu Al-Ghazali *Mwenyezi Mungu Apendezeshe sifa zake* akasema: “ama ustahiki wa utekelezaji wa hukumu haukuwa isipokuwa ni kwa yule Mwenye uumbaji na amri, kwani mtekelezaji wa hukumu ya Mfalme juu ya

(1) Kitabu cha Maqayis Al-Lugha “vipimo vya lugha”, 2/91, mada ya (حكم).

(2) Kamusi ya Lisanu Al-Arab 12/ 140 – 142 mada ya hukumu.

(3) Kitabu cha Ihkaam fi Usul Al-Ahkam “Hukumu katika misingi ya hukumu”
1/79.

anaowaongoza, hakuna Mfalme isipokuwa ni Muumba, hivyo hakuna hukumu wala amri isipokuwa ni kwake”⁽¹⁾.

Sehemu ya Pili: Maana ya Kukumu katika Haki ya Mwenyezi Mungu

Ndani ya Qurani limetumika neno mtoa hukumu kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na limekusudiwa ambapo limepokelewa kwa maana tatu:

Maana ya Kwanza: Hukumu ya Utungaji Sharia: Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: **«Hamuabudu badala yake ila majina tu mliyoyapanga nyinyi na baba zenu. Mwenyezi Mungu hakuyateremshia hayo uthibitisho wowote. Hapana hukumu ila ya Mwenyezi Mungu tu. Yeye Ameamrisha msimuabudu yeyote isipokuwa Yeye tu. Hiyo ndiyo Dini Iliyonyooka. Lakini watu wengi hawajui»**{Yusuf, 40}.

Hukumu hapa ni utungaji Sharia unaofungamana na Imami iliyopo juu ya kumpwekesha kwa nia safi, kauli yake Mola Mtukufu: **«Hapana hukumu ila ya Mwenyezi Mungu tu»** ni kubatilisha vitendo vyote vinavyoaminika kwa miungu yao.

Kwa maana, hakuna hukumu katika masuala ya Imani, Ibada, Mashirikiano (Matendeano) na katika kufaa kwake au kutofaa isipokuwa ni Mwenyezi Mungu Mtukufu peke yake, kwa sababu Yeye ndiye Muumba wa kila kitu, na Mjuzi pia wa kila kitu⁽²⁾.

Na Amesema Mwenyezi Mungu Utakasifu ni wake: **«Enyi mlioamini! Timizeni ahadi. Mmehalalishiwa wanyama wa mifugo, ila wale mnaotajiwa. Lakini msihalalishe kuwinda nanyi mumo katika Hija. Hakika Mwenyezi Mungu Anahukumu Apendavyo»**{Maidah, 01} .

Hapa hukumu ya Mwenyezi Mungu kwa maana ya uwekaji wake wa Sharia zinazofungamana na ahadi, mikataba, makubaliano na mfano wa hivyo, na kauli yake Mola Mtukufu: **«Hakika Mwenyezi Mungu Anahukumu Apendavyo»** kwa maana: Hakika Mwenyezi Mungu Aliyetukuka kwa sifa zake Anahukumu kwa waja wake vile Atakavyo ikiwa ni pamoja na kuhalalisha yale Anayotaka kuhalalisha na kuharamisha Anayotaka kuyaharamisha kama Apendavyo kwa mujibu wa hukumu na masilahi ambayo Anayajua Yeye Mwenye Utakatifu, basi tekelezeni makubaliano yake na ahadi zake wala mzivunje wala kuzipunguza⁽³⁾.

(1) Kitabu cha Al-Mustaswfiy, uk. 66.

(2) Tafsir Al-Wasiit ya Sheikh Mkuu wa zamani wa Al-Azhar Prof. Muhammad Sayyid Tantawy, 7/363.

(3) Tafasiri ya Al-Maraghy, 6/ 44.

Na hukumu ya Mwenyezi Mungu ya Kisharia ni taklifu kwa watu, basi mwenye kutekeleza amri zake na kujiepusha na makatazo yake, huyo atafaulu na kuwa na furaha, na mwenye kwenda kinyume na kupuuza amri hizo huyo atapata hasara duniani na Akhera.

Mola Mtukufu Amesema: **﴿Na ukikufikieni uongofu kutoka kwangu basi atakayeufuata uongofu wangu, hatapotea wala hatataabika ﴿ Na atakayejeiepusha na mawaidha yangu, basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki, na Siku ya Kiyama Tutamfufua hali ya kuwa kipofu﴾﴾**{Taha, 123: 124}.

Maana ya Pili: Hukumu ya Uwezo wa Kiulimwengu

Maana yake ni kuwa: Mwenyezi Mungu Amepitisha utaratibu na kanuni za ulimwengu ambazo zinahukumu viumbe hai kwa utashi wake Yeye Mwenyewe peke yake, wakati wowote Anapotaka hutokea, wala binadamu hawezi kubadilisha au kwenda kinyume nazo.

Mwenyezi Mungu Mtukufu Amesema: **﴿Je! Hawakuona kwamba Tunaifikia ardhi Tukiipunguza nchani mwake? Na Mwenyezi Mungu huhukumu, na hapana wa kupinga hukumu yake, naye ni Mwepesi wa kuhesabu﴾**{Ar-Raad, 41}.

Na Akasema tena: **﴿Sema: Mwenyezi Mungu Anajua zaidi muda waliokaa. Ni zake tu siri za mbingu na ardhi. Kuona kulioje na kusikia kwake! Hawana mlinzi isipokuwa Yeye, wala hamshirikishi yeyote katika hukumu yake﴾**{Al-Kahf, 26}.

Maana ya Tatu: Hukumu ya Akhera

Maana yake ni kuwa: Mwenyezi Mungu siku ya Kiyama huwahesabu watu kwa matendo yao watakaposimama mbele yake, na mwema kupata thawabu na muovu kuadhibiwa. Mola Mtukufu Amesema: **﴿Kisha watarudishwa kwa Mwenyezi Mungu, Mola wao wa Haki. Hakika, hukumu ni yake. Naye ni Mwepesi kuliko wote wanao hesabu﴾**{Al-An'aam, 62}.

Na Akasema tena: **﴿Sema: Ewe Mwenyezi Mungu! Muumba mbingu na ardhi! Mjuzi wa yasiyoonekana na yanayoonekana! Wewe Utahukumu baina ya waja wako katika waliyokuwa wakitofautina﴾**{Az-Zumar, 46}.

Sehemu ya Tatu: Matumizi ya Neno Hukumu kwa Mwanadamu

Umejifunza kwa yaliyopita kuwa Hakimu au Mwenye kuhukumu ni Mwenyezi Mungu Mtukufu, na ukasimamia kwenye maana ya kuhukumu kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa mujibu wa ilivyokuja na kupokelewa ndani ya Qurani Tukufu.

Swali: Je! Inafaa kutumika neno kuhukumu kwa mwanadamu yeyote?

Jibu: Ndiyo, kwani kuna Aya nyingi zimeegemeza utoaji hukumu kwa mwanadamu.

Mola Mtukufu Amesema: **﴿Ewe Daudi! Hakika Sisi Tumekufanya wewe uwe Khalifa katika nchi. Basi wahukumu watu kwa haki, wala usifuate matamano yakakupoteza kwenye Njia ya Mwenyezi Mungu﴾**{Sad, 26}.

Na Akasema tena: **﴿Na Daud na Suleiman walipokata hukumu katika kadhia ya konde walipolisha humo mbuzi wa watu usiku. Na Sisi Tulikuwa wenye kushuhudia hukumu yao hiyo ﴿ Tukamfahamisha Suleimani (kuliko mzee wake, Daudi). Na kila mmoja Tulimpa hukumu na elimu﴾**{Anbiyaa, 78: 79}.

Akasema tena Akiwa Anamwambia Mtume wake S.A.W: **﴿Hakika Sisi Tumekuteremshia Kitabu hiki kwa haki ili upate kuhukumu baina ya watu kwa Alivyokuonyesha Mwenyezi Mungu. Wala usiwe mtetezi wa makhaaini﴾**{An-Nisaa, 105}.

Ikiwa utasema: Aya za Qurani nilizozitaja zimeegemeza hukumu kwa Manabii wa Mwenyezi Mungu na Mitume wake, na hawa wamekingwa kwa Ufunuo wa Mungu, je umetuambia uwepo wa Aya zengine zilizoegemezwa hukumu ndani yake kwa wanadamu wote wasiokingwa na Ufunuo wa Mungu?

Nitasema: Ndiyo, Qurani Tukufu inakusanya Aya nyingi ambazo zimeegemeza hukumu kwa watu wasiokuwa Manabii, ikiwa utataka dalili ya hilo, basi soma kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu katika kuhukumu watu kwenye malipo ya kuua mnyama wakati wa mtu ameshahirimia Hija: **﴿Basi malipo yake yatakuwa kwa kuchinja kilicho sawa na alichokuwa, katika mifugo, kama wanavyohukumu waadilifu wawili miongoni mweni﴾**{Maidah, 95}.

Na Akasema tena katika kuhukumu kwao kwenye tofauti za mume na mke: **﴿Na mkichelea kuwepo mfarakano baina ya mke na mume basi pelekeni muamuzi kutokana na jamaa za mume, na muamuzi kutokana na jamaa za mke. Wakitaka mapatano Mwenyezi Mungu**

Atawawezesha. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Mwenye habari ﴿An-Nisaa, 35﴾.

Na Qurani ikawaita majaji kuwa ni mahakimu, Ikasema: **﴿Wala msiliane mali zenu kwa ubatilifu na kuzipeleka kwa mahakimu ili mpate kula sehemu ya mali ya watu kwa dhambi, na hali mnajua﴾** {Al-Baqarah: 188}.

Mwenyezi Mungu Akaisifu Dhati yake Takatifu kwa kauli yake Akimwambia Mtume wake S.A.W: **﴿Na wewe fuata yanayofunuliwa kwako kwa Wahyi. Na vumilia mpaka Mwenyezi Mungu Ahukumu, na Yeye ndiye Mbora wa mahakimu﴾** {Yunus: 109}.

Na kwa kauli yake kupitia ulimi wa Nabii Nuuh A.S: **{Na hakika ahadi yako ni haki. Na Wewe ni Mwenye haki kuliko mahakimu wote}** {Huud, 45}.

Aya zote hizo zinaweka wazi juu ya kufaa kutumika neno Hakimu au mtoa hukumu kwa Mwenyezi Mungu na kwa Wanadamu, lakini kwa maana mbili tofauti, wala hakuna mgongano kati ya maana hizo mbili kama vile matamshi mengine ambayo yanafaa kushirikiana.

Kutokana na hivyo, kuhukumu kunanasibishwa kwa Mtoa hukumu, na hucusudiwa Mola Mtukufu, na wakati mwengine hucusudiwa mtoa hukumu mwanadamu, na mtoa hukumu mwanadamu katika dunia ya watu huitwa Kiongozi au Khalifa au Amiri au Mfalme au Rais, majina yote haya ni ufahamu na uelewa mmoja nao ni kuongoza watu kwa Sharia ya Mwenyezi Mungu na kuendesha dunia kwa amri za Dini.

Sehemu ya Nne: Ufahamu wenye Makosa wa Aya za Hukumu kwa Namna Alivyoteremsha Mwenyezi Mungu na Ukosoaji wa Ufahamu huu na Kuchambua Shaka ya Msemaji wake

Katika historia ya Kiislamu halikufahamika neno kuhukumu isipokuwa ndani ya karne ya kumi na nne Hijria, na mtu wa kwanza kulitumia ni Abu Al-A'ala Al-Maududiy, na kutumika baada yake na Sayyid Qutub, na tokea hapo likaenea neno kuhukumu (*Hakimiya*) kati ya makundi ya Kiislamu wakimaanisha: Kumpwekesha Mwenyezi Mungu Mtukufu na hukumu, utunzi wa Sharia na Ufalme, na kukunjuliwa utungaji wote wa Sharia na mifumo kwake peke yake Mola Mtukufu, hivyo kuhukumu kwao ni kwa Mwenyezi Mungu tu peke yake, haifai kwa Mwanadamu vyovyote atakavyokuwa.

Anasema Abu Al-A'ala Al-Maududiy: “Hutumika neno hili - kwa maana kuhukumu - kwa Mamlaka kuu na Mamlaka zote, kwa mujibu wa kimsamiati wa kileo kwenye elimu ya Siasa”⁽¹⁾.

Na anasema: “Hakika sheria huanzishwa kwa utashi wa mwenye kuhukumu, na lazima kwa mtu kutii sheria hiyo, ama mwenye kuhukumu, hakuna sheria inayomfunga na kumlazimisha kumtii yeyote, yeye ndiye mwenye uwezo wa moja kwa moja na wala haifai kuulizwa kile alichokitungia sheria”⁽²⁾.

Kisha anaelezea kwa kusema: “Haifai kwa yeyote asiyekuwa Mwenyezi Mungu kutekelezwa hukumu yake kwa waja wa Mwenyezi Mungu kwa sababu hana haki hii isipokuwa ni Mwenyezi Mungu peke yake”⁽³⁾.

Sayyid Qutub amefuata mfano wake ambapo amesema: “Hakika hukumu haiwi isipokuwa ni kwa Mwenyezi Mungu, Yeye ndiye anayehusika kwa hukumu ya Uungu wake, ambapo kuhukumu ni katika sifa za Kiungu na mwenye kudai kuwa na haki katika hilo atakuwa amemvua Mwenyezi Mungu moja ya sifa ya Uungu wake ni sawa sawa akidai haki hii yake au ya tabaka fulani la watu au chama au taasisi au Umma au watu wote katika muundo uliopangiliwa kimataifa, na mwenye kumvua Mwenyezi Mungu sifa ya Uungu wake na kuidai basi atakuwa amemkufuru Mwenyezi Mungu kwa ukafiri wa wazi, na kukufuru kwake kutakuwa miongoni mwa mambo yanayojulikana kwa dharura katika Dini.

Na kudai haki hii hakuwi kwa sura moja ambayo humtoa mwenye kudai kwenye mzunguko wa Dini iliyonyooka, na kumfanya ni mwenye kumvua Mwenyezi Mungu katika moja ya sifa zake za Uungu wake, si katika muhimu kusema: **﴿Sijui kama mnaye mungu asiyekuwa mimi﴾** {Al-Qasas, 38}.

Au kusema: **﴿Mimi ndiye Mola wenu Mlezi mkuu kabisa﴾** {An-Naziat, 24}.

Kama alivyoyasema hayo Firauni kwa uwazi, lakini anadai haki hii na anamvua Mwenyezi Mungu kwa kuing'atua Sharia ya Mwenyezi Mungu kwenye kuhukumu na kutegemea sheria kutoka chanzo chengine.

Na kwa kusema tu kuwa upande ambao unamiliki kuhukumu, kwa maana ambao unakuwa ndio chanzo cha Mamlaka, upande mwengine

(1) Tadween Ad-Destuur Al-Islamy “Uandishi wa Katiba ya Kiislamu”, uk. 18.

(2) Marejeo yaliyopita, uk. 19.

(3) Marejeo yaliyopita, uk. 21.

usiokuwa wa Mwenyezi Mungu Mtukufu... hata kama itakuwa ni mkusanyiko wa Umma au mkusanyiko wa wanadamu”⁽¹⁾.

Na maelezo yaliyopita yanatuonesha kuwa kuhukumu kwa upande wa hawa watu ni katika misingi ya Dini na ni katika chanzo cha Imani, kisha kukosekana kutekelezwa kwake au kupingwa kunamaanisha ni ukafiri wa wazi, na wanatoa dalili juu ya hilo kwa kauli ya Mola Mtukufu: **«Na wasiohukumu kwa Aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio makafiri»** {Maidah, 44}.

Sayyid Qutub anasema kwenye tafsiri yake ya Aya iliyotajwa: “Kwa kauli hii iliyo wazi kabisa na kwa muenezo huu ambao unabebwa na herufi ya Kiarabu ya “Min” “من” ya sharti, na jibu la sentensi yake, ambapo inatoka kwenye mipaka iliyovaana na muda na sehemu, na kuchukua hukumu ya wote, kwa kila asiye hukumu kwa Aliyoteremsha Mwenyezi Mungu ndani ya kizazi chochote na kutoka upande wowote .. na sababu ndiyo ambayo tumeitaja .. nayo ni kuwa yule asiye hukumu kwa Aliyoteremsha Mwenyezi Mungu hakika anakuwa anapinga Uungu wa Mwenyezi Mungu, kwani Uungu ni katika sifa zake na hukumu zake ni kuhukumu Kisharia, na mwenye kuhukumu pasi na Aliyoteremsha Mwenyezi Mungu anapinga Uungu wa Mungu na sifa zake kwa upande mmoja, na kudai yeye mwenyewe kuwa ndiye mwenye haki ya Mungu na sifa zake kwa upande mwengine .. na nini kinapelekea kukufuru ikiwa si katika huyu wala yule?

Nini thamani ya madai ya Imani au Uislamu kwa ulimi na vitendo - navyo ni kielelezo chenye nguvu kuliko maneno - vinatamka ukafiri kwa ufasaha zaidi kuliko ulimi?”⁽²⁾.

Na kwa maelezo hayo inatuwiza wazi kuwa kuhukumu (*Hakemiya*) kwa upande wa watu hawa ni kuwa wanapinga hukumu ya mwanadamu, bali wanahitaji mapinduzi muhimu ya hilo, na kwa sababu hiyo wameanzisha mtazamo wa kisiasa katika Uislamu ili kuvua mamlaka, amri na utungaji Sharia kutoka mikononi mwa wanadamu, wala hawatoi ruhusa kwa yeyote miongoni mwao kutekeleza amri ya mwanadamu wa mfano wake na kumtii.

Mjadala wa Ufahamu huu wenye Makosa

Jambo la Kwanza: hakuna mgongano kati ya kutumia neno la mtoa hukumu kwa Mwenyezi Mungu na kwa wanadamu, ambapo kutumika huku ni kwa upande wa ushirikiano wa kitamko; tamko hili linatumika kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, kama vile inafaa kutumika kwa mwanadamu -

(1) Marejeo yaliyopita, uk. 4/1990.

(2) Kitabu cha Dhilal Al-Qurani (Kibuli cha Qurani), 2/898,

kama ulivyojifunza wakati wa kuzungumzia kwetu kuegemesha kuhukumu kwa Mwenyezi Mungu Mtukutu.

Ambalo tunataka kusisitiza hapa ni kuwa: mtoa hukumu katika wanadamu ni mtu asiye na kinga ya ufunuo anachaguliwa na watu wenye ututuzi na mfungamano, ambapo huitwa “Kwa msamiati wa kisasa upigaji kura wa moja kwa moja” na kuegemezewa hukumu yake kwenye vigezo vya lazima kufikiwa kama vile uadilifu na kushauriana, na jitihada zake katika kuanzisha sheria na Sharia ambazo zinahitajika na Umma wake katika wigo wa Sharia jumla zenye kukusanya sehemu zake jambo linalopelekea kuhukumu kwake kati ya wananchi wake kwa haki na uadilifu, na hali hii hawi mbishi wala mpingaji katika hukumu kuwa ukweli wake ni kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Na kwa maelezo haya inakubainikia kutokuwa sahihi dhana hii kwa wasemaji wake.

Jambo la Pili: Hakika katika kitu hatari kwenye ufahamu wa kuhukumu katika fikra za watu hawa ni hali ya mwanadamu ukilinganisha na Mungu, na ulinganishaji siku zote kati ya mfumo wa Mungu na mfumo wa mwanadamu, na katika mshangao mkubwa ikiwa tutajisalimisha na ufahamu huu basi mlango wa jitihada utafungwa mbele ya wabobezi katika elimu.

Ni namna gani na Maandiko ya Sharia yanahimiza juu ya kufanyia kazi kufikiri na mtazamo wa kina, hivi hakusema Mtume wa Mwenyezi Mungu S.A.W.: Kumwambia Muadh Ibn Jabal R.A. pale alipomtuma nchini Yemen “*Ni vipi utahukumu ikiwa utafikiwa na kadhia?*” akasema: *Nitahukumu kwa kutumia Kitabu cha Mwenyezi Mungu, akamuuliza: “Ikiwa hakuna ufumbuzi wake kwenye Kitabu cha Mwenyezi Mungu?” akasema: Nitaangalia kwenye Sunna za Mtume wa Mwenyezi Mungu, akamuuliza: Ikiwa hakuna kwenye Sunna za Mtume wa Mwenyezi Mungu wala kwenye Kitabu?” akasema: Nitajitahidi kwa mtazamo wangu, wala sitasita, Mtume S.A.W. akamgusa kifua chake na akasema: “Shukrani za Mwenyezi Mungu ambaye amemuwezesha Mjumbe wa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa yale yanayomridhisha Mtume wa Mwenyezi Mungu”⁽¹⁾.*

Je! Mtume wa Mwenyezi Mungu S.A.W. ambaye alimtuma mjumbe wake kuwa kadhi na hakimku kwa watu wa Yemen hakuridhia jitihada kwa kadhia isiyokuwa na Andiko? Bali Mtume S.A.W. alimuomba dua na kumgusa kifua chake akisema: “*Shukrani za Mwenyezi Mungu ambaye Amemuwezesha mjumbe wa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa yale yanayomridhisha Mtume wa Mwenyezi Mungu*”.

(1) Imetokana na Abu Daud katika Sunna yake ndani ya kitabu cha kadhia - mlango wa jitihada za rai katika hukumu, 3/302, Hadithi namba 3592.

Hivyo madai ya hawa ni madai mapana yanahitaji dalili, na dalili za kinyume chake, bali ikiwa utasalimisha kwao hilo litapelekea kukwamisha akili ya mwanadamu kufanya kazi zake katika kuinua maisha ya kifikra.

Jambo la Tatu: Ufahamu wa kuhukumu kwa namna hii unakuwa ni matumizi ya Dini kwa lengo la kufikia kwenye mamlaka na hukumu, halikadhalika kuhamisha mvutano wa kisiasa kuwa mvutano wa kidini unaruhusu udanganyifu mwamko wa Umma ili kufika kwenye kiti cha Utawala.

Sehemu ya Nne: Kauli yao: Mamlaka mikononi mwa wwanadamu ni ukafiri, inapingana na yaliyopitishwa katika misingi ya Uislamu kuwa jamii ndiyo inayomsimamia Kiongozi Mwislamu, nayo ndiyo inayomchagua na kumuondoa.

Na dalili yenye nguvu zaidi ni ya As-Siddiq R.A. katika hotuba yake ya kwanza baada ya kushika Ukhalifa: “Hakika yangu nimepewa usimamizi kwenu, wala sio mbora wenu, ikiwa nitafanya vizuri basi nisaidieni, na ikiwa nitafanya vibaya basi ninyoosheni”⁽¹⁾.

Sehemu ya Tano: Katika masilahi ya nchi kuna mambo yanahitaji uwekaji wa Sharia ambazo hazipo kwenye Aya za Qurani au kwenye Sunna, na hapa tunajiuliza: Kitu gani atafanya kiongozi kwenye mambo haya?

Na kwa sababu hii dalili za hukumu za Kisharia zilikuwa zenye kuegemea - baada ya Kitabu na Sunna - kwenye makubaliano ya wanachuoni, kisha Qiyasi kwa maana ya kuoanisha fatwa na matukio, kutafuta wema (upendeleo), masilahi ya Umma, mazoea na Sharia za waliotutangulia⁽²⁾.

Sehemu ya Sita: Utoaji wa dalili zao wa Aya kwenye Surat Al-Maidah juu ya kumkufurisha yule ambaye hajahukumu kwa vile Alivyoteremsha Mwenyezi Mungu, tunasema:

Mwanzo: Hakika kinachozingatiwa katika Imani ni kukubali moyoni na wala sio kutamka kwa ulimi, na hili ndiyo lililofikiwa na watu wa Sunna na Jamaa (Al-Asha'irah), na isiyokuwa kauli hii ambayo imepitishwa na Jopo la Wanachuoni wa Umma inakuwa ni kauli ya Khawarij ambao wamepitisha ukafiri kwa mtu asiyehukumu kwa vile Alivyoteremsha Mwenyezi Mungu kwa Waislamu, Wanachuoni wahikiki wamejibu hii kauli ya Khawarij, na kubainisha ubatilifu wake kwa sura tofauti amezitaja Imamu Fakhri Ar-Razy

(1) Kitabu cha Al-Bidaya wa An-Nihaaya (Mwanzo na Mwisho), 6/301.

(2) Rejea maana ya misamiati hii katika kitabu cha Misingi ya Sharia, miongoni mwa vitabu hivyo kwa mfano: Al-Mustasfa cha Imamu Ghazali, uk. 137 - 173, na kitabu cha hukumu katika msingi wa hukumu cha Imamu Al-Amady, 1/195, 3/173, 4/137.

Rehema za Mungu ziwe kwake kwenye tafasiri yake ya Aya kwenye Surat Maidah, akasema: “suala la pili: Wamesema watu wa Khawarij: Kila mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu basi huyo ni kafiri, na wakasema Wanachuoni wa Umma: Mambo hayapo hivyo, ama watu wa Khawarij wametoa hoja kwa Aya hii, wakasema: Yenyewe ni tamko kuwa kila mwenye kuhukumu tofauti na Aliyoteremsha Mwenyezi Mungu basi huyo ni kafiri, na kila mwenye kufanya dhambi anakuwa amehukumu kinyume na Aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, basi imelazimika kuwa kafiri.

Wazungumzaji na Wafasiri Wametaja Majibu Kuhusuuala hili

Jibu la Kwanza: Ni kuwa Aya hii imeteremka kwa Mayahudi, na yenye kuwahusu wao, na hoja hii ni dhaifu kwa sababu zingatia ni ujumla wa tamko na wala sio umaalumu wa sababu, na miongoni mwao wapo waliojaribu kuondoa swali hili, wakasema: Kusudio ni asiyehukumu miongoni mwa hawa ambao wametajwa kwa yale Aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ni makafiri, pia maelezo haya ni dhaifu, kwa sababu kauli yake: **«Na asiyehukumu kwa vile Aliyoteremsha Mwenyezi Mungu»** ni maneno ambayo ndani yake kumeingia herufi ya “Min” “من” ya sharti, na inakuwa kwa ujumla, na kauli ya mwenye kusema: Kusudio asiyehukumu kwa vile Aliyoteremsha Mwenyezi Mungu miongoni mwa wale waliotajwa, ni ongezeko katika andiko, na hilo halifai.

Jibu la Pili: Amesema Ataa: Huyo amekufuru pasi na ukafiri, na akasema Taus: Sio ukafiri unaomtoa kwenye mila kama yule anayemkufuru Mwenyezi Mungu na kupinga Siku ya Mwisho, kama kwamba wamebeba Aya juu ya kukufuru neema na wala sio kukufuru Dini, nayo pia ni hoja dhaifu, kwa sababu neno kukufuru likitumika linakwenda kwenye ukafiri katika Dini⁽¹⁾.

Jibu la Tatu: Amesema Ibn Al-Anbary: Inafaa kuwa maana: Na asiyehukumu kwa vile Aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, anakuwa amefanya kitendo kinacholingana na vitendo vya makafiri, na kwa sababu hiyo anafanana na makafiri, hoja hii pia ni dhaifu.

Jibu la Nne: Amesema Abdulaziz Ibn Yahya Al-Kinnany: Kauli ya Mwenyezi Mungu: **«Kwa vile Aliyoteremsha Mwenyezi Mungu»** ni mfumo jumla, na kauli yake: **«Na asiyehukumu kwa vile Aliyoteremsha Mwenyezi Mungu»** maana yake: Mwenye kuja kinyume na hukumu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: Katika kila Aliyoteremsha Mwenyezi Mungu,

(1) Ukafiri aina mbili: Ukafiri wa kuamini, na ukafiri wa neema, ukafiri wa neema tofauti na ukafiri wa Imani unakuwa haumtoi mtu kwenye Mila, amefasiri Imamu Bukhari katika sahihi yake katika kitabu cha Imani “Mlango wa kukufuru kwa watu, na amekufuru pasi na ukafiri”

basi hao ndio makafiri. Na hii ni kweli, kwa sababu kafiri ni yule ambaye amekwenda kinyume na hukumu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu katika kila Aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, ama mtu fasiki, yeye hakuja kinyume na hukumu ya Mwenyezi Mungu isipokuwa katika mambo machache, nayo ni matendo, ama Imani na kukiri anakubaliana nayo. Na hii pia ni dhaifu, kwa sababu lau ingekuwa Aya hii ni ahadi maalumu kwa mwenye kwenda kinyume na hukumu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu katika Aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, basi ahadi hii mbaya haijawagusa Mayahudi kwa sababu ya kwenda kinyume kwao na adhabu ya kumpiga mawe mzinifu, lakini Wafasiri wamekubaliana kuwa ahadi hii mbaya inawagusa Mayahudi kwa sababu ya kwenda kwao kinyume na hukumu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu katika tukio la kumpiga mawe mzinifu, inaonesha kudondoka kwa hili jibu.

Jibu la Tano: Ikrimah amesema: Kauli yake Mola: **«Na asiyehukumu kwa vile Alivyoteremsha Mwenyezi Mungu»** inamzungumzia mwenye kupinga kwa moyo wake, na kupinga kwa ulimi wake, ama mwenye kufahamu kwa moyo wake kuwa ni hukumu ya Mwenyezi Mungu na kukiri kwa ulimi wake isipokuwa yeye akaja na yaliyo kinyume chake, huyo anakuwa ni mwenye kuhukumu kwa vile Alivyoteremsha Mwenyezi Mungu Mtukufu, lakini ameacha hivyo wala halazimiki kuingia chini ya Aya hii, jibu hili ni sahihi, na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kujua zaidi⁽¹⁾.

Kutokana na maelezo hayo, asiyehukumu kwa vile Alivyoteremsha Mwenyezi Mungu akiwa ni mwenye kupinga kuwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu au akiwa ni mwenye kuamini kuwa ni hukumu isiyokuwa sahihi, au mwenye kucheza shere au kupinga, basi hakuna shaka kuwa ni kafiri.

Madamu Mwislamu anaamini kwa imani ya kweli kuwa Sharia ya Mwenyezi Mungu ni haki pamoja na kutopinga kwa moyo wake Sharia hii au kutoipinga kwa ulimi wake, basi haiwezekani kwa kiumbe yeyote atakayekuwa kumtoa kwenye mila ya Uislamu, na huzingatiwa kwa sababu ya upungufu huu kwa mujibu wa Sharia ya Mwenyezi Mungu kuwa ni Mwislamu aliyefanya maasi, na Mwislamu anayefanya maasi kwa watu wa Sunna ikiwa atatubu Mwenyezi Mungu hukubali toba yake, na akifa na msimamo wake juu ya dhambi yake pasi na kutubia, basi jambo litabaki kwa Mwenyezi Mungu.

Amesema mwenye kitabu cha Jawharah:

Mwenye kufariki bila ya kutubu dhambi zake

basi jambo linaachwa kwa Mola wake⁽²⁾.

(1) Tafasiri Al-Kabeer “Tafasiri kubwa” 12/6.

(2) Kitabu cha Jawhara Tawheed ukurasa 19.

Jibu la Sita: Kama vile katika kumkufurisha asiyehukumu kwa yale Alivyoteremsha Mwenyezi Mungu ni kwenda kinyume na muongozo wa Mtume wa Mwenyezi Mungu S.A.W., kutoka kwa Hudhaifah Ibn Al-Yaman R.A. amesema: *“Watakuja baada yangu Maimamu wasiofuata muongozo wangu wala kufuata Sunna zangu, na watakuwa miongoni mwao watu nyoyo zao ni nyoyo za mashetani ndani ya miili ya wanadamu, akasema Hudhaifah, nikauliza: Nitafanya nini Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu ikiwa nitawawahi watu hao? Mtume S.A.W. akasema: “Sikiliza na umtii kiongozi, hata kama utapigwa mgongo wako na kuchukuliwa mali zako, sikiliza na utii”*¹.

Imeonesha Hadithi kuwa uovu wa Kiongozi kutofuata muongozo wa Qurani na Sunna hazingatiwi ukafiri.

Baada ya haya tunajiuliza: Nini kusudio la Aya hii? Je! ni watu maalumu Aya imeteremka kwao, au kusudio la Aya ni jumla na sio watu maalumu?

Jibu: Ni kuwa kusudio la asiyehukumu kwa vile Alivyoteremsha Mwenyezi Mungu: Ni maalumu kwa Mayahudi, linajulisha hilo kwa mambo mawili:

Jambo la Kwanza: Ni sababu ya kuteremka kwake. na **Jambo la Pili:** Mtiririko wa Aya.

Ama sababu ya kuteremka kwake: Kuna Hadithi sahihi kuwa Aya hii imeteremka kwa sababu ya tukio la uzinifu lililofanywa na Myahudi, wakabadilisha hukumu ya Mwenyezi Mungu - nayo ni kupigwa mawe - ambayo imo ndani Taurati, na walikuwa wanataka Mtume S.A.W. awahukumie kwa hukumu nyengine.

Imetokana na Imamu Muslim kwenye Kitabu chake kutoka kwa Al-Barraa Ibn A'azib amesema: Alipitishwa mbele ya Mtume S.A.W. Myahudi sura yake ikiwa nyeusi⁽²⁾ akiwa na alama za kuchapwa viboko. Mtume S.A.W. akawaita na kuwauliza: “Hivi ndivyo ilivyo adhabu ya mzinifu ndani ya Kitabu chenu?” wakajibu: Ndiyo, akamwita mtu mmoja miongoni mwa Wanachuoni wa Kiyahudi na kumwambia: “Ninakuuliza kwa jina la Mwenyezi Mungu Ambaye Ameteremsha Taurati kwa Nabii Musa, hivi ndivyo ilivyo adhabu ya mzinifu ndani ya Kitabu chenu?” akasema, hapana, lau usingeniuliza hivi nisingekwambia, kuna adhabu ya kupigwa mawe, lakini mara nyingi imekuwa kawaida kwa wakubwa wetu, pindi tunapomshika mkubwa basi tunamwachia, na tukimshika mtu dhaifu basi tunamuadhibu kwa kitendo cha uzinifu, tukasema: Njooi tukubaliane

(1) Imetokana na Imamu Muslim katika kitabu chake cha mambo ya uongozi - mlango wa amri ya kulazimika kuwa na wengi wakati wa kutokea fitina na tahadhari ya walinganiaji kwenye ukafiri, 3/1476, Hadithi namba 1847.

(2) Angalia kitabu cha Nihayah fii ghariib Al-Hadithi 1/444

adhabu tutakayoitekeleza kwa mtu mtukufu na dhaifu, ndipo tukaweka adhabu ya kumpaka vumbi jeusi usoni lenye joto na adhabu ya kumchapa viboko badala ya kumpiga mawe. Mtume S.A.W. akasema: “Ewe Mwenyezi Mungu, hakika yangu mimi ndiye wa kwanza kuhuhisha amri yako pale wao walipoiuwa” akatoa amri Mtume S.A.W. yakupigwa mawe, ndipo Mwenyezi Mungu Mtukufu Alipoteremsha kauli yake: **«Ewe Mtume! Wasikuhuzunishe wafanyao haraka kukufuru»** mpaka kauli yake: **«Mkipewa haya basi yashikeni»** {Maidah, 41}. Kwani walisema: Nendeni Muhammad S.A.W., ikiwa atawaamrisheni mzinifu kumpaka vumbi jeusi usoni na kumchapa viboko basi chukueni amri yake, ikiwa atakupeni fatwa ya mzinifu kumpiga mawe, basi chukueni tahadhari katika hilo, ndipo Mwenyezi Mungu Mtukufu Akateremsha kauli yake: **«Na wasiohukumu kwa Aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio makafiri»**.

Akasema tena: **«Na wasiohukumu kwa yale Aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio madhalimu»**.

Na Akasema tena: **«Na wasiohukumu kwa yale Aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu basi hao ndio wapotofu»** {Maidah: 44, 45, 47}. Aya zote zimeteremka kwa makafiri⁽¹⁾.

Jibu la Saba: Ama mtiririko wa Aya, basi Aya imo ndani ya Surat Al-Maidah na umezungumzia watu wa Kitabu hasa Mayahudi, kama vile mpangilio wa Aya na zile zinazofuata zimezungumzia Mayahudi, mpangilio wake ni kauli ya Mola Mtukufu: **«Ewe Mtume! Wasikuhuzunishe wafanyao haraka kukufuru, miongoni mwa wanaosema kwa vinywa vyao: Tumeamini, na hali nyoyo zao hazikuamini, na miongoni mwa Mayahudi, wanaosikiliza kwa ajili ya uongo, wanaosikiliza kwa ajili ya watu wengine wasiokufikia. Wao huyabadilisha maneno kutoka pahala pake. Wanasema: Mkipewa haya basi yashikeni, na msipopewa haya tahadharini. Na mtu ambaye Mwenyezi Mungu Anataka kumfitini huwezi kuwa na madaraka naye mbele ya Mwenyezi Mungu. Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu hataki kuzitakasa nyoyo zao. Watakuwa na hizaya duniani, na Akhera watakuwa na adhabu kubwa»** Hao ni wasikilizaji kwa ajili ya kusema uongo, na ni walaji mno vya haramu! Basi wakikujia, wahukumu baina yao au jipuuze nao. Na ukijipuuza nao, basi wao hawatakudhuru kitu. Na ukiwahukumu, basi hukumu kati yao kwa uadilifu. Hakika Mwenyezi Mungu Anawapenda waadilifu» Na huwaje wakufanye wewe hakimu nao wanayo Taurati yenye hukumu

(1) Imepokelewa na Imamu Muslim katika kitabu cha mambo ya adhabu - mlango wa kupiga mawe Mayahudi watu wa dhimma katika utekelezaji wa adhabu ya uzinifu, 3/1327, Hadithi namba 1700.

za Mwenyezi Mungu? Kisha baada ya hayo wanageuka. Na hao si wenye kuamini ﴿Maidah, 41: 43﴾.

Na Aya zinazofuata ni kauli yake Mola Mtukufu: **﴿Na humo Tuliwaandikia ya kwamba roho kwa roho, jicho kwa jicho, pua kwa pua, sikio kwa sikio, jino kwa jino, na kwa majaraha kisasi. Lakini atakayesamehe basi itakuwa ni kafara kwake. Na wasiohukumu kwa yale Aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio madhalimu﴾** Na Tukawafuatishia hao Isa bin Maryamu kuyahakikisha yaliyokuwa kabla yake katika Taurati, na Tukampa Injili iliyomo ndani yake uongofu, na nuru na inayosadikisha yaliyokuwa kabla yake katika Taurati, na uongofu na mawaidha kwa wacha-Mungu⁽¹⁾.

Na kwa maelezo haya tunafahamu kuwa Aya zimeshuka kwa Mayahudi, na Mwenyezi Mungu Amewahukumu kwa ukafiri, kwa sababu walikataa hukumu ya Mola Mtukufu ndani ya Taurati: Ya kuwapiga mawe wazinifu na badala yake kutekeleza matakwa yao.

Kama itasemwa: Ikiwa Aya imeshuka kwa ajili ya Mayahudi, Je! inaweza kufanyiwa kazi kwa wasiokuwa Mayahudi miongoni mwa watu wa Sharia zengine ikiwa watafanya kama walivyofanya Mayahudi kwa kuhukumu pasi na Aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu?

Jibu: Wamesema kundi la Wanachuoni: Hukumu kwa wasiokuwa Mayahudi katika hilo ni kama hukumu kwa Mayahudi, kwa sababu mazingatio hapa ni upana wa amri (tamko) na wala sio uwepo wa sababu maalumu, na kwa vile Sharia za kabla yetu zimetuwekea Sharia sisi kwa yale yasiyokuwemo kwenye Sharia zetu yakiwa yasipingana nayo.

Na likasema kundi lengine la Wanachuoni: Hukumu hii ni maalumu kwa Mayahudi, na wasiokuwa wao wanahitaji hukumu nyengine, au kwa njia ya kulinganisha kwao, na vyovyote itakavyokuwa Aya siyo Andiko la kuwakufurisha Waislamu ikiwa hawatahukumu tofauti na Alivyoteremsha Mwenyezi Mungu, lakini pia haifai kuwa ni dalili, kwa sababu dalili pindi inapopewa uwezekano basi hudondoka kile kinachotolewa dalili, kwa maana haifai hoja kwa mdai, nayo hapa: Ni hukumu ya kumkufurisha Mwislamu ikiwa hatahukumu sawa na Alivyoteremsha Mwenyezi Mungu, kwani dalili ya dhana haikubaliki katika Imani kuthibitishia wala kukanushia⁽²⁾.

(1) Maidah: 45, 46. Na rejea kitabu cha Anwar Tanzeel, 2/128 na At-Tafseer Al-Kabeer, 12/6 na kitabu cha Rawh Al-Maany, 3/315.

(2) Rejea ubainifu kwa watu kutoka Al-Azhar Al-Sharif, 1/164 – 166.

Yaliyomo

Utangulizi	3
Kuhukumu (Hakimiya).....	6
Sehemu ya Kwanza :Ufahamu wa Kuhukumu Kilugha na Kimsamiati.....	7
Kuhukumu kwa upande wa lugha	7
Kuhukumu kimsamiati:.....	7
Sehemu ya Pili: Maana ya Kukumu katika Haki ya Mwenyezi Mungu	8
Maana ya Kwanza: Hukumu ya Utungaji Sharia	8
Maana ya Pili: Hukumu ya Uwezo wa Kiulimwengu:	9
Maana ya Tatu: Hukumu ya Akhera:	9
Sehemu ya Tatu: Matumizi ya Neno Hukumu kwa Mwanadamu	10
Mjadala wa Ufahamu huu wenye Makosa.....	13
Wazungumzaji na Wafasiri Wametaja Majibu Kuhusu suala hili.....	16



مشيخة الأزهر
مركز الأزهر للترجمة

Al-Azhar Center for Translation (ACT)